JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TUNDUMA

## HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA

Mhe. Mwenyekiti,
Mkutano wa baraza la madiwani,
**Halmashauri ya Mji Tunduma** **28.09.2022**

### YAH: MUHTASARI WA TAARIFA ZA HESABU ZA MWISHO ZA HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI 2022

### 1. UTANGULIZI

**Mhe: Mwenyekiti,**

Kwa mujibu wa Agizo Na. 31 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 na Kifungu 45(4) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa, 2000) inamtaka kila Afisa Masuuli kuandaa taarifa za mwisho za Hesabu na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi tarehe 30 Septemba au kabla ya tarehe hiyo kila mwaka. Kabla ya kuwasilishwa Taarifa hii inapaswa kujadiliwa kwenye Kikao cha Menejimenti ya Halmashauri, kikao cha Kamati ya Ukaguzi, Kamati ya Fedha na Utawala na kuthibitishwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani.Tayari taarifa hii imeshajadiliwa na kutolewa maoni katika Kikao cha Kamati ya Ukaguzi kilichofanyika tarehe 26.09.2022, kikao cha CMT Pamoja na kikao cha kamati ya fedha na utawala kilichofanyika tarehe 27.09.2022.

Kazi ya ufungaji hesabu za mwaka wa fedha 2021/2022 ilianza mapema mwezi Julai, 2022 na kwa sasa imeshakamilika tayari kwa ajili ya kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hesabu zilizoandaliwa zimezingatia Sheria za Fedha, Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 na kanuni zake za 2013, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa mwaka 2000 pamoja na viwango vya kimataifa vya uhasibu kwa sekta za umma.

### 2. TAARIFA ZA HESABU ZA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mhe: Mwenyekiti,**

Taarifa za Hesabu za Halmashauri zimetayarishwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta za Umma (IPSASs), pamoja na sehemu ya (iv) ya Sheria Na. 9 ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) Kulingana na Matakwa ya Agizo Na. 31(3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 Halmashauri imeandaa taarifa zifuatazo:-

1. Taarifa ya Mizania yaani "Financial Position". Uk. 4
2. Taarifa ya Mapato na Matumizi, yaani "Financial Perfomance". Uk. 116
3. Taarifa ya mabadiliko katika mali halisi za Halmashauri, "Changes in Net Assets" Uk. 127
4. Taarifa ya Mtiririko wa fedha, yaani "Cash Flow Statement". Uk. 126
5. Maelezo ya ziada (notes) yanayofafanua mambo muhimu yaliyopo katika Taarifa za Hesabu za Mwaka 2021/22.Uk. 117-125

## 3. MUHTASARI WA TAARIFA ZA HESABU ZA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mhe: Mwenyekiti,

Taarifa za Hesabu za Halmashauri ya Mji Tunduma kwa mwaka wa fedha 2021/2022 zimejumuisha Taarifa za Kifedha za Makao Makuu na taarifa za kifedha za ngazi zote za msingi zilizoko katika Halmashauri ya Mji kwa shughuli zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2021/2022. Taarifa hizo zinajumuisha Mapato, Matumizi, Mali za kudumu, Madeni, Mali zilizosalia katika Stoo na Salio la Fedha taslimu katika Akaunti za Halmashauri, Shule, Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali ya Mji na Kata. Mchanganuo wake ni kama unavyoonekana katika taarifa zifuatazo:-

### I: MIZANIA YA HALMASHAURI (STATEMENT OF FINANCIAL POSITION) (Uk.4)

Katika mizania ya Halmashauri ya Mji Tunduma, Taarifa zilizoainishwa ni kama ifuatavyo:-

### A: MALI ZA HALMASHAURI

i. **Mali za Muda Mfupi (Current Assets) zenye thamani ya TZS. 5,659,316,136**

Kipengele hiki hujumuisha mali za halmashauri zinazotegemea kutumika ndani ndani ya miezi kumi na Mbili baada ya tarehe 30/06/2022 ambazo ni:-

- Fedha taslimu (Cash and Cash Equivalent) Uk.5-7 — TZS 3,765,965,111
- Wadaiwa wa Halmashauri (Receivables) Uk.8-18 — TZS. 1,144,148,630
- Mali zilizosalia Stoo (Inventories) Uk.48-113 — TZS. 749,202,395

ii. **Mali za Kudumu (Non Current Assets) zenye thamani ya TZS. 36,607,542,934**

Kipengele hiki kinajumuisha mali za Halmashauri zinazotegemea kutumika kwa zaidi ya Miezi kumi na Mbili baada ya tarehe 30/06/2022. Mali hizi hujumuisha Ardhi, Majengo, Samani, Miundo mbinu ya Maji, Vifaa, Magari, Pikipiki, Baiskeli, Komputa, Mitambo, Mashine pamoja na Uwekezaji katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa.

Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

- Uwekezaji katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa — TZS. 36,000,000
- Mali (Ardhi, Majengo, Magari, Mitambo, Samani n.k) Uk.19-47 — TZS. 19,379,269,439
- WIP Uk.45-46 — TZS 17,192,273,496

### B: MADENI YA HALMASHAURI

i. **Madeni ya Muda Mfupi (Current Liabilities) yenye thamani ya TZS. 3,473,201,501**

Kipengele hiki kinajumuisha Wadai wa Halmashauri na Ruzuku ambayo haikutumika, mchanganuo wake ni kama ifuatavyo: -

- Wadai wa Halmashauri (Current Payables) Uk. 114-115 — TZS. 847,085,307
- Wadau katika Akaunti ya Amana — TZS. 2,177,276,663
- Madai ya Stahiki za Watumishi Uk. 128-130 — TZS. 72,908,179
- Bakaa ya Ruzuku ya Fedha za Matumizi ya Kawaida — TZS. 219,020,687

- Bakaa ya Ruzuku ya Fedha za Miradi — TZS. 2,588,638,772

**C: MALI HALISI ZA HALMASHAURI (NET ASSETS) Uk. 127**

a) **Mali Halisi za Halmashauri (Net Assets) yenye thamani ya TZS. 36,205,018,797**

Kipengele hiki hujumuisha Thamani ya Uwezeshaji wa Mali halisi za Halmashauri. Thamani hii hupatikana baada ya Kuchukua Mali za Halmashauri na Kutoa Madeni ya Halmashauri. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

- Mjumuisho wa Ziada (Accumulated Surplus) TZS. 36,169,018,797
- Akiba Nyingine (Other Reseve) TZS. 36,000,000

**II: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI (STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE) (Uk 116)**

Taarifa hii huonyesha mapato na matumizi ya Halmashauri ya Mji Tunduma kwa mwaka wa Fedha ulioishia 30 June 2022; Hulinganisha mapato na Matumizi ili kuona kama Halmashauri katika Utekelezaji wa Shughuli zake kwa mwaka umekuwa na Ziada (Surplus) au Upungufu (Deficity). Hali Halisi ni kama ifuatavyo:-

- Mapato kwa Mwaka TZS. 30,451,267,637
- Matumizi kwa Mwaka TZS. 18,008,898,355
- Ziada (Surplus) TZS. 11,645,018,511

**III: TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA (STATEMENT OF CASH FLOW) (Uk 126)**

Taarifa ya Mtiririko wa Fedha huonyesha namna Halmashauri ilivyopokea na kulipa fedha katika shughuli za Uendeshaji na Uwekezaji kwa Mwaka mzima na salio ishia la fedha Taslimu. Mchanganuo wake ni kama ifuatanyo:-

- Salio Anzia la Fedha (Cash & Cash Equivalents) TZS. 2,600,586,498
- Shughuli za Uendeshaji (Operating Activities) - Mapokezi TZS. 33,669,793,555
  Malipo TZS. (19,252,488,662)
- Shughuli za Uwekezaji (Investing Activities) - Malipo TZS. (13,182,237,178)
- Salio Ishia la Fedha Taslimu TZS. 3,765,965,111

**4. HITIMISHO**

**Mhe: Mwenyekiti,**

Kwanza kwa Umuhimu wa pekee naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wote wa mkutano wa baraza la madiwani ya Halmashauri kwa ushirikiano wa dhati mliotuonyesha katika kipindi chote cha maandalizi ya Taarifa hii. Nimategemeo yangu mtaendelea kutupatia ushirikiano katika kuijadili na kutoa mapendekezo ya maboresho ili kuleta matokeo chanya kwa Halmashauri.

Naomba kuwasilisha,

Dickson Mgawe
**Kny: MKURUGENZI WA MJI**
**TUNDUMA**